
# UKATILI DHIDI YA WANAWAKE KATIKA SIASA NA UCHAGUZI

## DHANA MUHIMU NA TAKWIMU



Tanzania, 2025

**Kitabu hiki kimetayarishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshugulika na Masuala ya Usawa ya Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake (UN Women) Tanzania kwa ushirikiano na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Africa (WiLDAF Tanzania).**


Maudhui yaliyomo katika kitabu hiki ni jukumu la UN Women Tanzania na WiLDAF Tanzania pekee, na hayawakilishi maoni ya wahisani, Bodi ya Utendaji ya UN Women, au Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa.

Kitabu hiki kimelenga kusaidia juhudi za kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa na Uchaguzi nchini Tanzania. Taarifa zilizowasilishwa hapa ni kwa madhumuni ya elimu, ushawishi wa sera na uhamasishaji, na hazipaswi kutafsiriwa kama msimamo wa kisheria au kisiasa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.



# UKATILI DHIDI YA WANAWAKE KATIKA SIASA NI NINI?

**Ukatili dhidi ya wanawake katika maisha ya kisiasa ni** tendo lolote au tishio la ukatili wa kijinsia linalosababisha madhara ya kimwili, kingono, au kisaikolojia kwa wanawake, na ambalo linazuia uwezo wao wa kutekeleza na kufurahia haki zao za kisiasa, iwe katika maeneo ya wazi au ya faragha. Haki hizi zinajumuisha:



- **Haki ya kupiga kura na kushika nafasi ya uongozi wa umma**
- **Kupiga kura kwa siri na kufanya kampeni kwa uhuru**
- **Kujiunga na kushiriki katika mikusanyiko**
- **Kufurahia uhuru wa maoni na kujieleza**



Chanzo: "Preventing Violence Against Women in Elections: A Programming Guide," UN Women na UNDP (2017)



# Sifa za Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa

**Ukatili dhidi ya wanawake katika siasa ni ukiukwaji wa haki za binadamu na shambulio la moja kwa moja dhidi ya ushiriki wao kidemokrasia. Unajitokeza kwa namna mbalimbali na huleta athari kubwa za kijamii na kisaikolojia, zikiwemo:**

- Kulenga wanawake wanaotekeleza haki zao za kisiasa
- Kulenga kunyamazisha sauti, mamlaka, na ushawishi wa wanawake kwa umma
- Kuathiri kwa makusudi ushiriki wa wanawake katika siasa kwa lengo la kuwakatisha tamaa au kuwaadhibu kwa kuingia katika ulingo wa masuala ya umma
- Kuwalenga wanawake kwa sababu ya jinsia yao
- Husababishwa na misingi ya mahusiano ya mamlaka yasiyo sawa kati ya wanaume na wanawake
- Hulenga kubatilisha mafanikio ya ushiriki wa wanawake katika siasa kwa kuwatisha wale wanaojitokeza, kugombea nafasi, kupiga kura au kushika Madaraka

**Tanbihi: Ukatili na unyanyasaji dhidi ya wanawake viongozi ni tishio kwa haki za binadamu na demokrasia. Matendo haya mara nyingi hufanywa na makundi yanayopinga ushiriki wa wanawake na yanayolenga kunyamazisha sauti zao katika siasa.**



# Nani Hufanya Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa?

Ukatili dhidi ya wanawake katika siasa (VAWP) hauhusiani na kundi moja tu, unaweza kufanywa na mtu binafsi, taasisi, au hata jamii nzima. Wafanyaji wa ukatili huu ni pamoja na:

- **Wanafamilia:** Wanaweza kuwakatisha tamaa au kuwaadhibu wanawake wanaoingia katika shughuli za umma, wakitumia sababu za kitamaduni au mila kandamizi.
- **Wanachama wa Vyama vya Siasa:** Wanaweza kuwanyanyasa, kuwapuuza, au kuwabagua wanawake ndani ya miundo ya chama chao.
- **Viongozi wa Vyama:** Wanaweza kuzuia maendeleo ya wanawake, kukataa kuwapatia rasilimali, au kutumia vitisho au kuwanyanyasa kingono ili kuwanyamazisha
- **Vyombo vya Habari:** Huchangia kupitia kuripoti kwa mtazamo unaopinga masuala ya jinsia, kuchafua sifa za wanawake, au kusambaza taarifa potofu.
- **Wawakilishi wa Serikali:** Wakiwemo maafisa wa vyombo vya usalama au viongozi wa serikali wanaoweza kutumia mbinu za kisheria au zisizo za kisheria kuzuia ushiriki wa wanawake katika siasa.
- **Watu Wasiofahamika:** Wanaweza kuwa watumiaji wa mitandao ya kijamii wanaotoa vitisho, matusi, au unyanyasaji dhidi ya wanawake, hasa katika majukwaa ya mitandao.
- **Jamii kwa Ujumla:** Shinikizo la kijamii, maneno ya kashfa, na kuabisha wanawake hadharani vinaweza kuwafanya wanawake kujitenga na kuacha kushiriki katika siasa.



# Je, Hii Ni Aina ya Ukatili au La?

**Katika jamii ya kidemokrasia, mijadala ya wazi na ukosoaji wa mawazo ya kisiasa, mitindo ya uongozi, na mapendekezo ya sera ni muhimu na yenye afya.**



**Majadiliano haya huimarisha utawala bora na kuchochea uwajibikaji. Hata hivyo, si kila aina ya mazungumzo ya kisiasa huwa salama, hasa pale yanapolenga watu binafsi kwa misingi ya jinsia badala ya uwezo au sifa.**

Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa (VAWP) hutokea pale ambapo wanawake wanashambuliwa, kudharauliwa, au kutengwa katika ushiriki wa kisiasa kwa sababu ya jinsia yao. Ukatili huu hauishii kwenye madhara ya kimwili pekee; unajumuisha madhara ya kisaikolojia, maneno ya kuumiza, tamaduni kandamizi, na mifumo ya kimfumo inayolenga kunyamazisha, kuwakatisha tamaa, au kupunguza uhalali wa wanawake katika uwanja wa kisiasa.

# Je, Hii Ni Aina ya Ukatili au La?



Kukosoa maamuzi ya sera, mtindo wa uongozi, au mikakati ya kisiasa ya mwanasiasa mwanamke; Kushiriki katika mjadala wa heshima kuhusu itikadi za kisiasa au mifumo ya utawala. Haya ni sehemu ya mchakato wa kidemokrasia na yanapaswa kutekelezwa kwa usawa kwa wagombea wote, bila kujali jinsia.

**SIO UKATILI** ✓

**Kuhoji uwezo wa mwanamke kuchaguliwa kwa misingi ya hali yake ya ndoa au familia:** Hii hupeleka mjadala kutoka kwenye sifa na uwezo wake hadi maisha yake binafsi, na hivyo kuendeleza mitazamo ya kijinsia inayomdhalilisha na kupunguza uhalali wake wa kisiasa.

**Kutumia nukuu au tafsiri za kidini kumkatisha tamaa au kumwondoa mwanamke katika ushiriki wa kisiasa:** Hii ni kutumia imani za kidini kama silaha ya kumtenga mwanamke, jambo ambalo mara nyingi huendeleza mfumo dume na kukiuka misingi ya usawa.

**Kutoa hoja za kijamii au kitamaduni kuhalalisha kutengwa kwa wanawake katika siasa:** Pale ambapo mila au desturi zinatumika kunyamazisha au kuwatenga wanawake, zinageuka kuwa chombo cha ukatili wa kimfumo kinachonyima haki yao ya kushiriki kikamilifu katika maisha ya umma.

**UKATILI** ✗

# Aina za Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa


KIMWILI

KISAIKOLOJIA

KINGONO

KIUCHUMI

# Aina za Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa



## Ukatili wa Kimwili

- Matumizi ya nguvu kwa makusudi ili kusababisha majeraha, madhara, au kifo
- Mauaji na vitisho vya mauaji
- Unyanyasaji wa kimwili na mateso
- Kupigwa, kushambuliwa, au kushambuliwa kwa kutumia nguvu
- Kukamatwa na kuzuiliwa bila sababu za msingi
- Kusambaratisha mikusanyiko kwa kutumia nguvu
- Kuweka vikwazo dhidi ya uhuru wa kutembea au kusafiri
- Kutekwa nyara
- Kupotezwa kwa lazima (kutoweka bila maelezo, mara nyingi kwa sababu za kisiasa)

# Aina za Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa



## Ukatili wa Kisaikolojia

- Unyanyasaji wa maneno na mashambulizi ya kihisia
- Vitisho vya madhara na vitisho vya kunyamazisha
- Kutishwa, kutengwa, au kubaguliwa
- Unyanyasaji wa maneno kutokana na maamuzi ya kisiasa
- Kudhihakiwa, kuaibishwa, na kusambaziwa uvumi
- Kulazimishwa kupiga kura kwa chaguo la familia au kwa shinikizo
- Uwakilishi hasi katika vyombo vya habari
- Unyanyasaji wa mtandaoni (kwa matusi, vitisho, au kejeli)
- Vitisho vya talaka au kuvunjika kwa ndoa kutokana na ushiriki wa kisiasa
- Vikwazo vya maadili kutoka kwa viongozi wa kidini au wa Mila
- Kutengwa na jamii kwa sababu ya msimamo wa kisiasa

# Aina za Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa

## Ukatili wa Kingono

- Njia zisizotakiwa za kumtongoza mwanamke au kuomba upendeleo wa kingono
- Unyanyasaji wa kingono
- Unyonyaji wa kingono
- Rushwa ya ngono
- Kulazimishwa kutoa huduma za kingono ili kupata fursa au kinga (sextortion)
- Tabia za maneno au vitendo vya kingono visivyotakiwa
- Ubakaji unaofanywa kwa sababu za kisiasa kama chombo cha vitisho na ugaidi
- Shambulio na unyanyasaji wa kingono unaolenga kumdhibiti, kumtisha, kumdhalilisha, na kumnyima haki ya kushiriki
- Kusambaza picha mnato au mjongeo za kingono kwa lengo la kuchafua



## Ukatili wa Kiuchumi

- Uharibifu wa mali
- Kukataliwa mshahara au fedha stahiki
- Kukataliwa fursa ya kupata rasilimali za kifedha, ikijumuisha zile za kifamilia
- Kukataliwa rasilimali za kampeni
- Ugawaji usio wa haki wa rasilimali
- Kutengwa katika upangaji wa bajeti na mipango ya kifedha
- Kulazimishwa kuchangia fedha kwa ajili ya kampeni za viongozi wa chama
- Kukataliwa fedha za ruzuku kwa wawakilishi wa Viti Maalum na kulazimishwa kufanya kampeni kwa ajili ya kura za majimbo

# Aina Zinazojitokeza Mara kwa Mara za Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa



Wanawake wanaoshiriki katika siasa hukumbana na aina mbalimbali za ukatili, ambapo zile zinazojitokeza mara kwa mara ni:

- **Ukatili wa kisaikolojia na wa kingono:** Hii inajumuisha matusi ya maneno, kushambuliwa kwa tabia au sifa binafsi, na matendo ya kingono yasiyotakiwa, iwe katika maeneo ya wazi au ya faragha, yanayolenga kunyamazisha na kuwatisha wanawake.
- **Vitisho vinavyolenga familia zao, juhudi za kuwatenga kijamii, na mashambulizi dhidi ya maadili yao ya kibinafsi:** Haya huathiri hadhi ya wanawake na kuwakatisha tamaa kushiriki katika siasa.
- **Unyanyasaji wa kingono ndani ya vyama vyao vya siasa au kudhalilishwa kwa namna ya kijinsia:** Wanawake wanaweza kunyimwa heshima, kutendewa kwa dharau, au kulazimishwa kukabiliana na mazingira ya kisiasa yasiyo salama kwa sababu ya jinsia yao.



# Makundi ya Wanawake Wanaokumbwa na Ukatili Katika Siasa

- Wagombea wanawake
- Viongozi wanawake walioko madarakani
- Wapiga kura wanawake
- Waandishi wa habari wanawake
- Wanafamilia wa wanawake wanaoshiriki siasa
- Watetezi wa haki za binadamu wanawake
- Wanaharakati wanawake wa asasi za kiraia
- Watendaji na waangalizi wa uchaguzi wanawake
- Watumishi wa umma na maafisa wa serikali wanawake
- Wafuasi wa vyama vya siasa na wafanyakazi wa kampeni wanawake



**Tanbihi:** Wanawake wanaoshiriki katika siasa na ambao wanakabiliwa na aina nyingi na zinazovuka mipaka za ubaguzi, kwa misingi ya kabila, dini, ulemavu, au hali nyingine, hulengwa kwa kiwango kikubwa na ukatili, unyanyasaji, na vitisho.

# TAKWIMU ZINASEMAJE?

**Kwa bahati mbaya, ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na maeneo ya umma ni jambo linachukuliwa la kawaida na limeenea kwa kiwango kikubwa.**

- **Asilimia 80** ya wabunge wanawake waliripoti kukumbwa na ukatili wa kisaikolojia, ikijumuisha kudhalilishwa, vitisho, na kauli za kibaguzi wa kijinsia.
- **Asilimia 67** walikumbana na tabia za kibaguzi wa kijinsia, mara nyingi kutoka kwa wenzao wa kiume, hasa wale kutoka vyama pinzani.
- **Asilimia 42** walipokea vitisho vya kuuawa, kubakwa, au kutekwa nyara, hasa kupitia majukwaa ya mtandaoni.
- **Asilimia 40** walikumbwa na unyanyasaji wa kingono, na asilimia 23 walipitia ukatili wa kimwili.
- Wanawake walio chini ya umri wa miaka 40, wasio na ndoa, wenye ulemavu, na kutoka makundi madogo ya kijamii walilengwa kwa kiwango kikubwa zaidi.
- Wabunge wanawake wanaotetea usawa wa kijinsia na haki za wanawake walikuwa katika hatari zaidi ya kukumbwa na ukatili.
- Mabunge mengi hayakuwa na mifumo salama ya kuripoti ukatili au kutafuta msaada.

**Chanzo:** *IPU, Sexism, Harassment and Violence Against Women in Parliaments in Africa (202*



# TAKWIMU ZINASEMAJE?



## Unyanyasaji wa Kingono Katika Vyumba vya Habari

Utafiti uliofanywa mwaka 2023 na TAMWA kwa kushirikiana na International Media Support (IMS) ulibaini kuwa:

- **Asilimia 77** ya wafanyakazi wanawake wa vyombo vya habari walikumbwa na unyanyasaji wa kingono ndani ya taasisi zao za habari.
- **Asilimia 27** waliripoti kunyanyaswa na vyanzo vya habari au wakati wakitekeleza majukumu yao kazini.
- **Asilimia 59.4** ya watoa taarifa muhimu walithibitisha kuwa unyanyasaji wa kingono na rushwa ni mambo ya kawaida katika vyumba vya habari nchini Tanzania.

**Chanzo:** *TAMWA, 2023*

# UKATILI DHIDI YA WANAWAKE KATIKA UCHAGUZI NI NINI?

Ukatili dhidi ya wanawake katika uchaguzi (VAWE) unahusisha tendo lolote au tishio la ukatili linalolenga wanawake kwa sababu ya jinsia yao na nafasi yao katika mchakato wa uchaguzi. Hii inajumuisha wanawake kama wapiga kura, wagombea, maafisa wa uchaguzi, wanachama wa vyama vya siasa, au wanaharakati wa kisiasa.



**Sifa za Ukatili dhidi ya Wanawake Katika Uchaguzi**

- VAWE ni ukatili unaolenga jinsia ya mtu: Si ukatili wa kisiasa tu, bali ni ukatili unaolenga kunyamazisha wanawake, kuwaadhibu kwa kushiriki, au kuwakatisha tamaa kushiriki katika maisha ya umma.
- Unaweza kuwa wa kimwili, kingono, kisaikolojia, au kiuchumi: Kuanzia mashambulizi na unyanyasaji hadi vitisho, kuchafuliwa kwa sifa, na kunyimwa rasilimali za kampeni.
- Hutokea katika maeneo ya wazi na ya faragha: Kituoni wakati wa kupiga kura, mtandaoni, majumbani, au ndani ya vyama vya siasa.
- Unadhoofisha demokrasia: Kwa kuzuia ushiriki wa wanawake, VAWE huharibu uadilifu wa uchaguzi na kuzuia utawala jumuishi.

**Chanzo;** *UNDP; Preventing violence against women in Elections: A programming guide, December 2017*

# Takwimu zinasemaje Kuhusu VAWE?

**Jukwaa la Wanawake wa Vyama Mbalimbali Tanzania (TWCP)** lilifanya uangalizi wa temati katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, likilenga hasa Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Uchaguzi (VAWE). Matokeo yao yalionyesha kuwa:

- **Asilimia 16** ya waangalizi walishuhudia mashambulizi dhidi ya wanawake katika mikutano ya kisiasa.
- **Asilimia 18** walipokea taarifa kuhusu mashambulizi hayo.
- **Asilimia 45** ya matukio yaliyoripotiwa yalihusisha ukatili wa kisaikolojia, kama vile unyanyasaji wa maneno.
- **Asilimia 30** yalihusisha mbinu za vitisho na kuwatisha wanawake.

Kwa mujibu wa ripoti ya **CWHRDs ya mwaka 2020**, wagombea wanawake na wanaharakati walikumbana na aina mbalimbali za ukatili nchini Tanzania, zikiwemo:

- **Ukatili wa kisaikolojia:** Matusi ya maneno, kuchafuliwa kwa sifa, na vitisho, hasa wakati wa mikutano ya kampeni na kwenye majukwaa ya mtandaoni.
- **Unyanyasaji wa kingono:** Kuguswa bila idhini na kauli za kudhalilisha kutoka kwa wenzao wa kiume na wanachama wa vyama vya siasa.
- **Vitisho:** Vitisho vya kuuawa, kubakwa, au kulazimishwa kujiondoa kwenye kugombea nafasi.
- **Ukatili wa kiuchumi:** Kukataliwa fedha za kampeni, kuhujumiwa kwa rasilimali, na kutengwa na msaada wa chama.
- **Unyanyasaji wa mtandaoni:** Kusambazwa kwa taarifa za uongo, picha binafsi bila idhini, na unyanyasaji wa moja kwa moja kupitia majukwaa kama WhatsApp na Telegram.



**Vyanzo:**

- CWHRDs, Ripoti ya Uangalizi wa Uchaguzi, 2020
- TWCP, Ripoti ya Uangalizi wa Uchaguzi, 2015

## Jinsi Wanawake Wagombea Wanavyolengwa Wakati wa Uchaguzi

- Kutukanwa, kudhihakiwa, kushutumiwa kwa ukosefu wa maadili au kuwasilishwa kwa taswira hasi kutokana na maamuzi yao ya maisha binafsi, hasa wakati wa mikutano ya kampeni na mahojiano ya vyombo vya Habari, ili kuharibu taswira yao ya umma.
- Kuguswa bila idhini, kufuatwa kwa nia mbaya, na kunyanyaswa (mtandaoni na ana kwa ana), au kutolewa kauli za kudhalilisha kutoka kwa wanaume na wanawake, ikiwemo wenzao, wanachama wa vyama, au wapiga kura.
- Kampeni za upotoshaji, unyanyasaji wa picha, kusambaza uvumi wa kashfa, kuchafua sifa, na vitisho kupitia majukwaa kama WhatsApp, Instagram, X (Twitter), Facebook, TikTok, na Telegram.
- Kukataliwa kupata fedha za kampeni au msaada wa chama, kutengwa katika mijadala ya umma, matukio ya hadhara, na vipindi vya televisheni, na hivyo kulazimika kujifadhili au kujiondoa kwenye kinyang'anyiro.
- Kupokea vitisho vya madhara ya kimwili, ubakaji, au kutengwa kijamii endapo wataendelea na kampeni au kuzungumzia masuala ya usawa wa kijinsia.
- Kutopewa nafasi au kuepukwa katika mchakato wa ndani wa uteuzi wa chama, kukataliwa au kuwekwa pembeni licha ya kuwa na sifa stahiki.
- Imani za muda mrefu zinazopinga uongozi wa wanawake, ambapo baadhi ya jamii huona kugombea kwa mwanamke kuwa ni jambo lisilofaa au la kuaibisha.
- Kupewa ahadi ya kuteuliwa kwenye Viti Maalum ili wajiondoe kwenye kugombea majimbo.
- Wanawake kuondolewa katika mchakato wa uteuzi wa chama.
- Wanawake kuzuiwa kujisajili kugombea nafasi katika majimbo ya uchaguzi.



# Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa na Uchaguzi Hutokea Lini?

**VAWP na VAWE si matukio ya mara moja, huambatana na wanawake katika safari yao ya kisiasa. Vipindi muhimu ambapo ukatili huongezeka ni pamoja na:**

- **Wanapokuwa katika nafasi ya uongozi ndani ya chama cha siasa:** Hii inaweza kujumuisha kuhujumiwa na wenzao wa kiume wanaokataa kutambua uongozi wao, kutengwa katika maamuzi muhimu ya chama hata wanaposhika nyadhifa rasmi, au kunyanyaswa na wanachama, hasa wanapothibitisha mamlaka yao.
- **Baada ya kuteuliwa kuwa wagombea wa chama:** Hii hujumuisha kampeni zinazolenga maadili yao, maisha ya kifamilia, au muonekano wao; vitisho vya mtandaoni na ana kwa ana; na shinikizo kutoka kwa viongozi wa chama au jamii kujiuzulu "kwa ajili ya mshikamano" au kwa sababu za kitamaduni.
- **Wakati wa mchakato wa uteuzi na kampeni:** Hii hujumuisha kuvurugwa kwa matukio ya kampeni yanayoongozwa na wanawake, upendeleo wa vyombo vya habari na uwasilishaji wa taarifa potofu, unyanyasaji wa mtandaoni ikiwemo kufichua taarifa binafsi (doxing), matusi ya kingono, na upotoshaji wa makusudi.



# Mielekeo ya Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa na Uchaguzi (VAWP/VAWE)

| Mwelekeo | Mwelekeo | Aina ya Ukatili | Watenda Ukatili |
|---|---|---|---|
| **Shughuli ya Kisiasa na Ngazi ya Uchaguzi** | Wagombea Ubunge wa Majimbo/Kata | Ukatili wa Kisaikolojia | Wagombea na wanachama wa Upinzani |
| | Wagombe Ubunge wa Viti Maalum | Ukatili wa Kingono | Viongozi wa Chama |
| | Ngazi ya Jimbo | Ukatili wa Kisaikolojia | Wanachama wa Upinzani na Jamii |
| | Ngazi ya Kata | Ukatili wa Kisaikolojia; Ukatili wa Kimwili zaidi | Wanajamii zaidi |
| | Shughuli za kisiasa ndani ya Chama | Unyanyasaji na Unyonyaji wa Kingono na Ukatili wa Kiuchumi. | Viongozi wa Chama |
| | Shughuli za Kisiasa nnje ya Chama | Ukatili wa kimwili na Kisaikolojia | Wagombea wa upinzani na wanajamii |
| **Sifa Binafsi za Mgombea** | Umri/Uzoefu – Mabinti wasionauzoefu | Ukatili wa kingono, rushwa ya ngono, unyonyaji wa kingono zaidi | Viongozi wa chama na wanachama wakongwe |
| | Umri/Uzoefu – Wanawake wazoefu | Ukatili wa Kiuchumi na kisaikolojia zaidi | Viongozi wa Chama, wanajamii, wapinzani |
| | Elimu-Elimu ndogo | Ukatili wa Kingono | Viongozi wa Chama |
| | Elimu Kubwa | Ukatili wa Kiuchumi na kisaikolojia zaidi | Viongozi wa Chama |
| | Hali ya Uchumi- Mdogo | Ukatili wa Kingono | Viongozi wa Chama, familia na Wenza |
| | Hali ya Uchumi-Kubwa | Ukatili wa Kiuchumi na Kisaikolojia | Viongozi wa Chama |
| | Hali ya Ndoa-Waloolewa | Ukatili wa Kisaikolojia na Kiuchumi zaidi | Viongozi wa Chama, familia na Wenza |
| | Hali ya Ndoa- wasioolewa | Ukatili wa Kingono na Kisaikolojia | Viongozi wa Chama |
| **Muktadha/ Mazingira** | Maeneo ya Umma | Ukatili wa Kimwili, Kisaikolojia na Kingono | Polisi na Wapiga kura |
| | Maeneo ya Nyumbani | Ukatili wa Kiuchumi na kisaikolojia zaidi | Mume na wanafamilia |
| | Office za Vyama | Ukatili wa Kingono na Kiuchumi zaidi | Viongozi wa Chama |
| | Maeneo mengine | Ukatili wa Kisaikolojia | Wafanyakazi wenzake katika chama |
| | Kwenye Mitandao ya Kijamii | Ukatili wa Kisaikolojia na Kingono | Watumiaji wa mitanda0 ke na me |

# Athari za Muda Mrefu za Ukatili Dhidi ya Wanawake Katika Siasa

- Wanawake hukatishwa tamaa kugombea nafasi za uongozi
- Wanasiasa wanawake hushauriwa au kushinikizwa wasiseme hadharani
- Baadhi ya wanawake huamua kujiondoa kabisa katika siasa
- Sauti za wanawake hukosekana katika mijadala ya umma kuhusu sheria na sera
- Vijana wa kike na wanawake kutoka makundi yaliyotengwa huogopa kushiriki katika siasa
- Wanasiasa wanawake hupunguzwa uhalali wao wa kisiasa
- Huchangia mgawanyiko wa kijamii na kisiasa
- Hufanya ukatili dhidi ya wanawake katika maeneo ya umma na kisiasa kuonekana kama jambo la kawaida
- Huzuia uhuru wa wanawake kutoa sauti zao za kisiasa



# Mambo Ambayo Mamlaka za Serikali Zinaweza Kufanya Kukabiliana na VAWE/VAWP

- Kupitisha sheria mpya au kapitia upya, na kutekeleza sheria zilizopo zinazofanya ukatili dhidi ya wanawake katika siasa kuwa kosa la jinai, kutoa msaada, ulinzi na kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa wahanga.
- Kuweka mifumo ya ufuatiliaji na utoaji taarifa kuhusu VAWE/VAWP na kuunganisha na miundo iliyopo (wasaidizi wa kisheria, mashirika ya wanawake, asasi za kiraia, Dawati la Jinsia la Polisi, na kamati za MTAKUWWA)
- Kutoa mafunzo yenye mtazamo wa kijinsia kwa vyombo vya usalama, ikiwemo Tume za Uchaguzi, ORPP, Jeshi la Polisi, na PCCB
- Kuweka kanuni za maadili kwa taasisi za serikali na/au vyama vya siasa
- Kutunga na kutekeleza kanuni za Tume ya Uchaguzi kwa ajili ya kuzuia na kushughulikia ukatili
- Kusaidia Tume za Uchaguzi kuingiza masuala ya kijinsia katika miundo ya kiutendaji na majukumu ya usimamizi
- Kukusanya takwimu kuhusu kiwango cha ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi ili kuchagiza mabadiliko ya sera na kupima matokeo.
- Kuweka mwongozo wa kitaifa wa taratibu za uteuzi wa Viti Maalum kwa vyama vyote vya siasa



# Mambo Ambayo Wagombea na Vyama vya Siasa Wanaweza Kufanya Ili Kuzuia VAWE/VAWP

- Kuheshimu **Kanuni za Maadili** zinazokataza ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi, kwa wagombea na wanachama wa vyama
- Kuandaa sera, kanuni na taratibu zinazoonyesha **kutovumilia kabisa ukatili dhidi ya wanawake** katika siasa na uchaguzi
- Kuhamasisha na kushawishi sheria na sera zinazolinda wanawake na watu walioko kwenye mazingira hatarishi dhidi ya ukatili.
- Kuimarisha mifumo ya ndani ya kukabiliana na ukatili, kama vile **Madawati ya Jinsia ya Chama na Kamati za Maadili**
- Kuandaa **mafunzo kwa wagombea, timu za kampeni, na wafanyakazi wa chama** kuhusu ukatili dhidi ya wanawake katika siasa
- Kuhamasisha ushirikishwaji na uwakilishi wa wanawake na makundi yaliyotengwa ndani ya mifumo yao, ili kuchagiza utungaji wa sera zinazozingatia hali halisi na zenye mwitikio wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake katika siasa.
- Kulaani waziwazi ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi, na kuhamasisha jamii kwa kuonyesha ukubwa wa tatizo hilo, madhara yake, pamoja na umuhimu wa kuvunja unyanyapaa na ukimya unaozunguka suala hilo.
- **Kutoa taarifa ya matukio ya ukatili** dhidi ya wanawake katika siasa kwa mamlaka husika
- Kujikita katika **kujadili mafanikio na sera za wanasiasa wanawake**, badala ya maisha yao binafsi au muonekano wao



# Mambo Ambayo Vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii Vinapaswa Kufanya Ili Kuzuia VAWE/VAWP

- Kutumia mbinu za kuripoti Habari zenye mtazamo wa kijinsia na zinazomlenga manusura, kabla, wakati, na baada ya uchaguzi
- Kuepuka kutengeneza au kusambaza habari zinazowasilisha wanawake kwa kutumia mitazamo ya kijinsia au lugha ya kibaguzi
- Kutoa taarifa ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi kwa mamlaka husika
- Kutoa mafunzo kwa wahariri na waandishi kuhusu mbinu za kuripoti zenye kuzingatia usawa wa kijinsia na masuala yanayohusiana na ukatili dhidi ya wanawake kwenye siasa
- Mitandao ya kijamii iondoe taarifa potofu na vitisho dhidi ya wanawake wanaoshiriki katika siasa na uchaguzi
- Kutoa muda sawa wa matangazo kwa wanasiasa wanawake na wanaume
- Kuonyesha kutovumilia kabisa aina yoyote ya kuripoti inayochochea au kuendeleza ukatili dhidi ya wanawake katika siasa
- Kupinga na kusahihisha taarifa potofu na upotoshaji unaolenga wanasiasa wanawake, kabla, wakati, na baada ya uchaguzi
- Chapisha hadithi mbalimbali ili kuhamasisha jamii kuhusu ukatili dhidi ya wanawake katika siasa, kwa kuonyesha ukubwa wa tatizo hilo, madhara yake, na umuhimu wa mabadiliko ya kijamii ili kuvunja unyanyapaa na ukimya.



# Mambo Ambayo Watu Binafsi Wanapaswa Kufanya Ili Kuzuia VAWE/VAWP



- Kutoa msaada na kuhamasisha wanawake kugombea nafasi za uongozi wa kisiasa
- Kukemea mitazamo ya kibaguzi wa kijinsia dhidi ya wanasiasa wanawake katika mijadala ya faragha na ya umma
- Kuwakilisha kwa usawa takwimu za kisiasa za wanawake bila upendeleo
- Kuepuka kuwashambulia wanawake katika maisha ya umma kwa misingi ya muonekano wao, hali ya kifamilia, au hadhi ya kijamii
- Kuripoti matukio ya ukatili dhidi ya wanawake katika siasa kwa mamlaka husika
- Kutetea kwa mamlaka za mitaa na kitaifa kupitisha sheria mpya na kutekeleza zilizopo
- Kutumia mitandao ya kijamii na majukwaa mengine kuchukua hatua dhidi ya ukatili dhidi ya wanawake katika siasa na uchaguzi
- Kuonyesha mshikamano na kuunga mkono wanawake waathirika wa ukatili wa kisiasa
- Kuepuka kusambaza taarifa potofu dhidi ya wagombea na wanasiasa wanawake

# Mambo Ambayo Asasi za Kiraia zinapaswa Kufanya Ili Kuzuia VAWE/VAWP

- Kuandaa kampeni za kuelimisha jamii kuhusu VAWP/VAWE na athari zake kwa demokrasia
- Kutumia redio, mitandao ya kijamii, na simulizi za maisha kubadili mitazamo hatarishi ya kijinsia na kuhamasisha uongozi wa wanawake
- Kufuatilia, Kukusanya na kuchapisha takwimu kuhusu matukio ya ukatili dhidi ya wagombea wanawake, wanaharakati, na wapiga kura
- Kushirikiana na vyombo vya habari na mashirika ya uangalizi kufichua mifumo ya ukatili na kuwawajibisha wahusika
- Kutoa msaada wa kisheria, ushauri wa kisaikolojia, na maeneo salama kwa wanawake waliokumbwa na ukatili wa kisiasa
- Kuunda mitandao ya rufaa na watoa huduma za afya, polisi, na dawati la jinsia
- Kuhamasisha na kushawishi kupitishwa kwa sheria mpya, au kupitia upya na kutekeleza sheria zinazofanya ukatili dhidi ya wanawake katika siasa kuwa kosa la jinai.
- Kushinikiza kupitishwa kwa sheria madhubuti na mifumo ya utekelezaji inayotambua VAWP kama kosa la jinai
- Kushirikiana na Bunge, Tume za Uchaguzi, na vyama vya siasa kuhimiza sera zenye mtazamo wa kijinsia
- Kutoa ushauri na msaada kwa wagombea wanawake, hasa vijana na wanawake kutoka makundi yaliyotengwa
- Kuimarisha nguvu ya Pamoja katika kupaza sauti za wanawake katika maamuzi ya kisiasa
- Kujumuisha viashiria vya ukatili dhidi ya wanawake katika shughuli za uangalizi wa uchaguzi
- Kutoa taarifa ya matukio ya ukatili dhidi ya wanawake katika siasa kwa mamlaka husika.



# Mifumo ya Kisheria ya Kuwalinda Wanawake Wanaokumbwa na Ukatili Katika Siasa

- Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 **inakataza aina yoyote ya ubaguzi**, jambo linaloashiria pia **marufuku ya ukatili dhidi ya wanawake katika siasa**. Katiba hii inatoa msingi imara wa, **Usawa wa kijinsia, Haki za binadamu na Ulinzi dhidi ya ukatili na unyanyasaji** Kwa kutumia tafsiri pana ya vifungu vinavyohusu usawa na haki za binadamu.



# Mifumo ya Kisheria ya Kuwalinda Wanawake Wanaookumbwa na Ukatili Katika Siasa

| Ibara | Muhtasari wa Ibara husika | Namna gani Inakataza VAWP |
| --- | --- | --- |
| **Ibara ya 12(1) & (2)** | Binadamu wote huzaliwa wakiwa huru, sawa, na wana haki ya heshima na utu. | Katiba inalinda wanawake wanaoshiriki katika siasa dhidi ya matendo ya kudhalilisha, unyanyasaji, na ukatili kwa kuthibitisha usawa wa utu. |
| **Ibara ya 13(1)** | Usawa mbele ya sheria, watu wote ni sawa mbele ya sheria bila ubaguzi. | Katiba Inahakikisha ulinzi wa kisheria kwa wanawake dhidi ya vitisho vya kisiasa, kutengwa, na ukatili. |
| **Ibara ya 13(5)** | Inafafanua maana ya ubaguzi (jinsia, kabila, dini, mtazamo wa kisiasa, n.k. ni sababu zilizokatazwa). | Katiba Inakataza moja kwa moja ubaguzi wa kijinsia, ikijumuisha unyanyasaji wa kisiasa au ukatili unaolenga wanawake. |
| **Ibara ya 21(1)** | Kila raia ana haki ya kushiriki katika uongozi wa nchi. | Katiba Inathibitisha haki ya wanawake kupiga kura, kufanya kampeni, kugombea, na kushiriki katika siasa bila hofu au vikwazo. |
| **Ibara ya 66(1)(b)** | Inatoa nafasi maalum za uwakilishi kwa wanawake ndani ya Bunge ili kuhakikisha ushiriki wao. | Katiba Inaimarisha ushiriki wa wanawake katika siasa na kupunguza vikwazo vya kimfumo vinavyochochea ukatili wa kisiasa. |
| **Ibara ya 81** | Inampa Tume ya Uchaguzi mamlaka ya kuweka taratibu kwa vyama vya siasa katika uteuzi wa Wabunge chini ya Kifungu cha 66(1)(b). | Katiba Inalinda uteuzi wa wanawake katika viti maalum kwa kuhakikisha taratibu za vyama ni wazi, za haki, na zinazopunguza hatari ya hujuma, kutengwa, au unyanyasaji. |

# Mifumo ya Kisheria ya Kuwalinda Wanawake Wanaokumbwa na Ukatili Katika Siasa

*Makosa mengi ya Ukatili dhidi ya wanawake yana sura ya Jinai, hivyo mengi yamepigwa marufuku katika Sheria Ya Makosa ya Jinai*

| Aina ya Ukatili | Kosa | Vifungu vya Sheria |
|---|---|---|
| **a) Ukatili wa Kimwili** | Kupigwa au Shambulio la Kimwili | inajulikana kama "madhara ya Mwili" – Kanuni ya Adhabu Sura ya 16: Vifungu vya a 225 na 228(1) |
| | Shambulio | Kanuni ya Adhabu Sura ya 16: Vifungu vya 240–243 |
| | Utekaji nyara | Kanuni ya Adhabu Sura ya 16: Vifungu vya 245–256 |
| | Mauaji | Kanuni ya Adhabu Sura ya 16: kifungu cha 196 |
| **b) Ukatili wa Kingono** | Unyanyasaji wa Kingono | Kanuni ya Adhabu Sura ya 16: kifungu cha 135(3); na Kanuni za Maadili ya Uchaguzi 2025 |
| | Shambulio la Aibu | Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kifungu cha 135(1) |
| | Ubakaji | Kanuni ya Adhabu Sura ya 16: kifungu cha . 130 |
| | Rushwa ya Ngono na Vitisho vya Kingono | Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya, 329: Kifungu cha 25 |
| | Tuhuma za kuchafua/ Kashfa | Inaweza kushtakiwa kwa makosa ya Madai, Lakini pia Kanuni za maadili ya Uchaguzi, 2025 imekataza. |

# Mifumo ya Kisheria ya Kuwalinda Wanawake Wanaokumbwa na Ukatili Katika Siasa

*Makosa mengi ya Ukatili dhidi ya wanawake yana sura ya Jinai, hivyo mengi yamepigwa marufuku katika Sheria Ya Makosa ya Jinai*

| Aina ya Ukatili | Kosa | Vifungu vya Sheria |
|---|---|---|
| **c) Ukatili wa Kisaikolojia** | Vitisho | Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 |
| | Lugha za Chuki | Inaweza kushtakiwa kwa makosa ya Madai, Lakini pia Kanuni za maadili ya Uchaguzi, 2025 imekataza |
| | Ukatili wa Mtandaoni/ | Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni), 2020 – Tangazo la Serikali Na. 538/2020, Kanuni ya 16, Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 (Cybercrimes Act, 2015) |
| | Kuchafua sifa ya Mtu | Kanuni za maadili ya Uchaguzi, 2025 imekataza |
| | **Matumizi mabaya yanayohusiana na uhalifu wa mtandaoni:,** Uonevu wa mtandaoni (Cyberbullying), Uchapishaji wa taarifa za uongo Ujumbe usiotakiwa, Ukiukaji wa faragha | Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 (Cybercrimes Act, 2015, Kifungu cha 16, 20, 23, 24, |

# Mifumo ya Kisheria ya Kuwalinda Wanawake Wanaokumbwa na Ukatili Katika Siasa

*Makosa mengi ya Ukatili dhidi ya wanawake yana sura ya Jinai, hivyo mengi yamepigwa marufuku katika Sheria Ya Makosa ya Jinai*

| | Kosa | Kifungu cha Sheria |
|---|---|---|
| **Makosa ya Uchaguzi** | **Vitendo vya ukiukaji:**<br>• Vitisho<br>• Shurutisho<br>• Vitisho vya hofu (intimidation)<br>• Rushwa<br>• Upigaji kura kwa udanganyifu (personation)<br>• Kuzuia mchakato wa uchaguzi<br>• Matumizi ya nguvu au vurugu<br>• Kauli za uongo dhidi ya wagombea<br>• Tabia zisizo za nidhamu kwenye kampeni<br>• Vitisho katika vituo vya kupigia kura<br>• Utovu wa nidhamu na matumizi mabaya | **Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, 2024:**<br>• **Kif. 87**: Ushawishi usiofaa – vitisho, shurutisho, vitisho vya hofu<br>• **Kif. 88**: Rushwa – udanganyifu wa kiuchumi<br>• **Kif. 89**: Upigaji kura wa udanganyifu (Personation) – kupiga kura kwa jina la mtu mwingine / kujifanya mtu mwingine<br>• **Kif. 90**: Kuzuia mchakato wa uchaguzi – unyanyasaji dhidi ya wagombea/wapiga kura<br>• **Kif. 91**: Matumizi ya nguvu au vurugu – mashambulizi ya mwili, hasa dhidi ya wagombea wanawake<br>• **Kif. 92**: Kauli za uongo dhidi ya wagombea – kashfa, mashambulizi ya tabia<br>• **Kif. 93**: Tabia zisizo za nidhamu kwenye kampeni – matusi, vitisho, vurugu za mikutano<br>• **Kif. 94**: Vitisho kwenye vituo vya kupigia kura – ukandamizaji wa wapiga kura kwa misingi ya kijinsia<br>• **Kif. 135**: Marufuku ya Ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia |

# Mifumo ya Kisheria ya Kuwalinda Wanawake Wanaokumbwa na Ukatili Katika Siasa

*Makosa mengi ya Ukatili dhidi ya wanawake yana sura ya Jinai, hivyo mengi yamepigwa marufuku katika Sheria Ya Makosa ya Jinai*

| Mtoa Huduma | Namba ya Mawasiliano Bure | Aina ya Msaada |
|---|---|---|
| Jeshi la Polisi | 112 | **Mwitikio wa dharura kwa ukatili wa mwili, vitisho na unyanyasaji wa uchaguzi** |
| TAKUKURU | 113 | **Kutoa taarifa za rushwa, hongo, na matumizi mabaya ya madaraka katika uchaguzi** |
| Msaada kwa Wanawake na Watoto | 116 | **Msaada kwa manusura wa ukatili wa kijinsia (GBV) kwa wanawake na watoto, ikiwemo ukatili wa kisiasa** |
| WiLDAF Tanzania (Msaada wa Kisheria) | 0800 780 070 | **Msaada kwa manusura wa ukatili wa kijinsia (GBV) kwa wanawake na watoto, ikiwemo ukatili wa kisiasa**<br>**Msaada wa kisheria bila malipo, msaada wa kisaikolojia, na rufaa za dharura kwa manusura wa GBV** |
| WiLDAF Tanzania (Msaada wa Kisheria) | 0685 559 954 | **Mawasiliano mbadala ya simu kwa dharura** |
| WiLDAF Tanzania (Msaada wa Kisheria) | 0624 475 478 | **Namba ya msaada wa ziada kwa msaada wa kisheria na kisaikolojia** |

UN WOMEN

WiLDAF TANZANIA